




Na Rais
Russell M. Nelson



“MUWEKENI
YESU KRISTO
KWANZA.
KWA SABABU
MAISHA YENU
YA MILELE
YANATEGEMEA
IMANI YENU
KWAKE.

Rais Russell M. Nelson



UJUMBE WA MKUTANO MKUU KUTOKA KWA NABII

Mpango wa Ajabu wa Baba wa Mbinguni

Mpango wa Baba wa Mbinguni kwa ajili yetu ni wa *ajabu*. Ni nini tunachofanya katika maisha haya ambacho kweli ni muhimu. Upatanisho wa Mwokozi ndiyo kitu kinachoufanya mpango wa Baba wa Mbinguni uwezekane.

Mwokozi aliteseka ili kwamba Yeye aweze kutufariji, kutuponya, na kutuokoa katika nyakati za uhitaji. Kwa sababu ya Upatanisho usio na mwisho wa Yesu Kristo, mpango wa Baba yetu wa Mbinguni ni mpango mkamilifu! Unamruhusu kila mmoja *wetu* kuchagua *jinsi* tutakavyoishi.

Ninawaalikeneni muanze “**kufikiria selestia**”! Wakati unapokuwa na shida, fikiria selestia! Wakati unapojaribiwa na majaribu, fikiria selestia! Wakati maisha au wapendwa wako wanapokuangusha, fikiria selestia!

Unapofikiria selestia, utataka kusali zaidi na kwa dhati. Utayaona majaribu katika njia mpya. Wakati unapofikiri selestia, imani yako itaongezeka.

Mungu yu hai. Yesu ndiye Kristo. Kanisa Lake limerejeshwa ili kuwabariki watoto wote wa Mungu. ●



Kufikiria selestia:

kuwa mwenye kufikiria mambo ya kiroho na kufuata mfano wa Mwokozi

Umetoholewa kutoka kwenye “Fikiria Selestia!” Liahona, Nov. 2023, 115–17.

W/OO/WI KWA YESU, NA MICHAEL, WALIM



FIKIRIA Selestia!

Rais Nelson alifundisha kwamba kufikiria selestia kunaweza kutusaidia kufanya chaguzi nzuri. Katika kila jua, chora au andika kitu ambacho wewe ungeweza kufanya ili kufuata mfano wa Mwokozi.

